

Uchanganuzi wa Matini za Kifeministi katika Taarab Teule

¹Mary Mugasia Malenya, ²Sheila Pamela Wandera-Simwa

¹Kaimosi Friends University College, Kenya

²Laikipia University, Kenya

Abstract

*This paper examines language as a social construct through feminist analysis of selected taarab songs. A lot of research has been done on taarab majoring on various elements like language use, ideology and power, characteristics of taarab and themes but little has been done on taarab and feminism. This research intended to fill this gap by analyzing selected taarab songs from a feminist perspective in order to identify the social role of women through the language used. The study utilized the following objectives: to analyze tropes used in the selected songs; to discuss feminist issues as revealed in the selected songs; and to identify the role of women in selected taarab songs. This research employed the African Feminism Theory, as it was apt in discussing feminist issues and the role of women in society. The researcher used descriptive research design. Purposive sampling was used to identify taarab songs that bear tropes, feminist themes and defined the role of women in society. The songs selected included **Sina Muda Huo** by Leila Rashid and **Chози la Mama** by Mzee Yusuf. Primary data was collected from music albums that contained the selected songs. This was done by listening to the songs and identifying specific taarab verses which were later transcribed and analyzed according to the objectives. Secondary data was collected from published books, journals and newspapers from the libraries and online sources. Collected data was classified, organized, analyzed and interpreted and the results presented qualitatively. Results and recommendations were presented in accordance with research objectives, research questions and theoretical tenets. The outcome of the research was intended to benefit researchers on feminism theory who want data on the role of women in society and those who will want to do more research on feminism.*

Keywords: Feminist texts, gender roles, language, social practice, tarab genre.

Ikisiri

Makala hii inanalenga kuangalia lugha kama tendo la jamii kupitia kwenye uchanganuzi wa matini katika nyimbo teule za taarab kwa kuzingatia mtazamo wa kifeministi. Madhumuni ya makala hii ni kuchanganua semi ambazo zimetumika katika nyimbo teule za taarab, kudhihirisha namna masuala ya kifeministi yanavyojitokeza katika taarab na kujadili namna lugha inayotumika katika nyimbo za taarab inavyomchora mwanamke na kumjukumisha katika jamii ikilinganishwa na mwanamume. Nadharia inayotuongoza katika utafiti huu ni Ufeministi kutokana na jinsi inavyojadili masuala ya ufeministi na inavyojaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Makala hii basi inajadili kuwa mwelekeo na mtazamo wa jamii kuhusu uhusiano baina ya mwanamke na mwanamume huibuliwa katika lugha inayotumiwa na wasanii kupitia semi. Wasanii wa taarab huwa ni wabunifu ambao huweza kucheza na sanaa ya lugha katika kuelezea uhalisia ndani ya jamii. Data za makala hii zilikusanywa kwa kuchanganua nyimbo mbili zilizoimbwa na bendi ya Jahazi Modern Taarab (JMT) nchini Tanzania. Nyimbo hizo ni Sina Muda Huo ulioimbwa na Leyla Rashid na Chози la Mama ulioimbwa na Mzee Yusufu. Pia mtafiti alisikiliza kanda zenye nyimbo za taarab teule alizonunua madukani kwa lengo la kukusanya data mwafaka. Data iliyokusanywa, ilifanyiwa unukuzi, iliainishwa, kupangwa, kuchanganuliwa na kufasiriwa kulingana na mihimili ya nadharia.

Maneno muhimu: Lugha kama tendo la jamii, majukumu ya kijinsia, matini za kifeministi, taarab.

Utangulizi

Waswahili wameenzi matumizi ya nyimbo katika sherehe za harusi, mazishi, unyago na jando, kuzaliwa kwa mtoto au kupewa jina. Tangu kale walikuwa na sherehe za michezo mbali mbali, kazi, mashindano katika kukariri mashairi na kadhalika (Yego, 2011). Nyimbo za taarab tangu mwanzo ziliimbwa katika maeneo ya burudani ambapo watu walizichepukia kwa kuzipenda sana. Hadi sasa lugha inayotumika katika nyimbo hizo ni ya mahaba na huwa imeshamiri ufumbaji kwa lengo la kubana maneno fulani yanayoweza kusikika kimatusi endapo yataimbwa waziwazi. Watunzi wa taarab wanazingatia matumizi ya tamathali za semi ambapo baadhi ya semi hizo huchukua maana zinazohitaji uchanganuzi wa kina ndipo zipate kueleweka.

Mapitio ya Maandishi

Kwa jumla baadhi ya kazi za Fasihi ya Kiswahili zimemchora na kumuweka mwanamke katika hadhi ya chini ikilinganishwa na wanaume. Katika hali hii (Nyenyeembe, 1997: 14) anasema:

Waandishi wengi wa kazi za fasihi iwe kwa kukusudia au kwa kutokusudia wameziandika kazi zao ili kuliridhisha soko lao, yani wanaume ambapo wametia chumvi nyingi mno katika kumwelezea mwanamke, hata kuharibu picha sahihi ya mwanamke.

Naye (Omari, 2009) anataja baadhi ya sifa mbaya za mwanamke zinazotajwa katika kazi za fasihi ambazo ni watu wasio waaminifu, watu wenye uwezo mdogo kiakili, watu wasiojali, wazini na malaya. Taswira za aina hii zinapatikana katika muziki wa Bongo Flewa. Kwa mfano kuna taswira za mwanamke kama malaya na mtu anayetumiwa kutimiza matakwa ya kingono ya wanaume. Taswira hizo huenda si zao la wasanii pekee, bali ni kiwakilishi cha fikra na mtazamo wa jamii kuhusu dhana ya mwanamke. Mwanamke anapewa majina mbalimbali katika muziki kama vile mtoto, baby, demu, kipusa, ua, shangingi, ndege, tausi, kiburudisho na kifaa. Utafiti huu japo umejishughulisha na muziki wa Bongo Flewa umetufaa kwa sababu makala yetu imechunguza masuala ya jinsi na jinsia sawa na yaliyoshughulikiwa humu ila tumetumia mtazamo wa kifeministi kuchunguza muziki teule wa taarab huku Omari akichunguza taswira ya mwanamke katika muziki wa Bongo Flewa.

Lugha katika riwaya imetumika kumdunisha mwanamke hivi kwamba mwanamume amepewa nafasi ya juu zaidi katika kutekeleza majukumu mbali mbali huku mwanamke akisalia na uwezo mdogo wa kujikomboa au hata bila namna yoyote ya kumuwezesha kujikwamua. Haya ni maoni yake (Halliday, *epics*, 1985) ambaye amechunguza dhamira na uteuzi wa msamiati ili kudhihirisha usawa uliopo kijinsia. Halliday anakubaliana na Matei ambaye amechunguza mahusiano ya kijinsia katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Matei amebaini kwamba mahusiano ya kijinsia yapo na yamemsawiri mwanamke kama kiumbe aliye mnyonge kwa mujibu wa taasubi ya kiume. Utafiti wake umetufaa katika kuelewa namna mwanamke anavyosawiriwa na wasanii mbali mbali na kuwa mojawapo wa vyanzo vya utetezi wa haki za mwanamke (Matei, 2014).

Kwa uyaakinifu, makala hii inajadili uchanganuzi wa matini kifeministi katika nyimbo teule za taarab. Ni nyimbo ambazo zimetumika katika kuwaleta wanawake wa jamii ya Waswahili pamoja (Timammy, 2002). Nyimbo hizi zina sifa za kimaeneo, kiutunzi, lugha na maudhui. Taarab ni neno la kiarabu lenye maana ya furaha kulingana na kamusi ya kiarabu ya *Al Faraid Al Durriya* na linatokana na neno lingine *tariba* ambalo pia ni la kiarabu. Neno hili lina visawe vingine kama vile yatiribu na taraba (Askew, 2002). Taarab ni muziki wa Waafrika wa Pwani uliopokea athari kutoka tamaduni nyingi hasa muziki wa Waarabu na Wahindi. Nyimbo za taarab zinakisiwa kuimbwa mara ya kwanza kule Zanzibar na kwamba

zililetwa huko na Waarabu wakati wa utawala wa Sultan Sayyid Barghash (Khatib, 1992). Jamii ya Waswahili imekuwa na salua ndefu yenye mtagusano mkubwa na jamii nyingine za watu kutoka maeneo tofauti ulimwenguni. Wageni wengi waliowahi kutoka mataifa ya Uingereza, Ureno, Uarabuni, Ugiriki, Uchina na Uitaliano walichangia uwepo wa maingiliano makubwa kupitia kwenye nyenzo za ndoa. Waswahili wakaoa na kuolewa na wageni na hivyo ndoa zikachukua mwelekeo wa mchanganyiko kati ya wenyeji na wageni. Maingiliano zaidi yakatokea kwenye biashara ya watumwa, biashara ya pembe za ndovu na dini. Maingiliano ya kibiashara na kidini yalichipua utamaduni wa Waswahili kuathirika hadi sasa na mseto wa mila na desturi kutoka maeneo ya kigeni kote ulimwenguni. Mabadiliko mengi yalitokea katika matumizi ya lugha ya Kiswahili huku lugha za kigeni zikiingiliana na lugha ya wenyeji.

Muziki wa taarab ulichezwa na kupata umaarufu mkubwa katika jamii ya Waswahili kipindi hiki. Hadi sasa nyimbo za taarab hutungwa mara nyingi na wanaume na wanawake wanakuwa waimbaji katika bendi mbalimbali (Massamba, 2002). Baadhi ya hizo nyimbo zimetamalaki maudhui yanayomlenga mwanamke kwa kueleza sifa zake kwa namna ya kumdunisha, kumkejeli, kumsuta na kumwonyesha kama mwenye umbea, masengenyo, masimango na dharau. Lugha ya mafumbo hutumika kama mbinu ya tasfida lakini pia ni mbinu ya kuendeleza itikadi (Fairclough, 1989). Maudhui yanayotawala katika nyimbo za taarab ni matokeo ya matukio katika maisha: Masuala ya mapenzi, itikadi za jamii, mahusiano ya kijamii, mitindo ya maisha ya kila siku na uozo katika jamii. Zipo nyimbo nyingine za taarab ambazo zinamsifu mwanamke na kusisitiza apewe heshima pamoja na kueleza majukumu anayoyatekeleza katika jamii ambayo ni ya muhimu na magumu kutekelezwa na wanaume.

Nyimbo za taarab huwa na mikakati fiche inayotumika kubadilisha mahusiano ya kijamii na kiuchumi (Zaja, 2008). Zaja amechunguza namna mambo yanayostahili kuwa fiche katika nyimbo za taarab yameanza kuwekwa peupe na wasanii. Hata hivyo amejikita katika utunzi, kurekodi na kusambaza nyimbo hizo na ameonyesha kwamba japo mwanamke amewekwa pembeni, kushiriki kwake katika uimbaji, kurekodi na pia kutunga nyimbo hizo anatomia nafasi hiyo kukinza itikadi ya taasubi ya kiume yaani ubabedume bila ufahamu wa wanaume wanaowapa nafasi ndogo na hafifu katika masuala ya siasa, uchumi na jamii. Makala hii imechanganua baadhi ya matini ambayo imetumika kimafumbo ili maana ipate kueleweka kiuhalisia kama tendo muhimu la lugha katika jamii kwa kujikita kwenye mtazamo wa kifeministi. Baadhi ya hizo nyimbo zimetamalaki maudhui yanayomlenga mwanamke kwa kueleza sifa zake mbalimbali kwa namna ya kumdunisha, kumkejeli, kumsuta na kumwonyesha kama mwenye umbea au dharau. Tumezichanganua kiufeministi tukirejelea nadharia ya ufeministi kwa jumla ambayo inachunguza na kujaribu kutatua matatizo yanayoikumba jinsia ya kike katika jamii iliyo na wingi wa taasubi ya kiume. Jambo hili linadhihirika katika taswira ya mwanamke katika nyimbo mbalimbali na pia katika jamii ya Kiafrika kwa jumla kama tunavyoonyesha hapa chini.

Taswira ya Mwanamke katika Nyimbo za Dini

Nyimbo za dini katika karne hii ya ishirini na moja zimetumiwa na baadhi ya wasanii katika kuendeleza maudhui yanayomchora mama kama kiumbe mvumilivu hususan katika malezi. Msanii Bonny Mwaitege anamsawiri mama kama mtu ambaye anapitia shida nyingi anapowalea watoto. Anasema kuwa hana uwezo wa kumlipa kwa yale ambayo anatenda ila nikumuomba Mama Baraka kutoka kwa Mungu. Katika wimbo wake wa *Mama Mama* anasema:

Mama Mama Mama
Uwezo wa kukulipa sina

Kwa taabu ulininyonyesha
Namuomba Mungu akupe Baraka Mamaaa....

Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva

Taswira ni dhana itumiwayo kutoa maelezo yanayounda picha fulani akilini mwa msomaji wa kazi ya fasihi (Wamitila, 2003). Taswira ni utumiaji wa lugha unaoibua hisia za msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi kutokana na picha aipatayo akilini mwake baada ya kusoma au kusikiliza kazi za kifasihi. Kwa kawaida kila jamii huwa na ishara mbalimbali. Baadhi ya ishara hizo hutumiwa na wasanii katika kazi za kisanii. Ishara hizo zilizozoeleka katika jamii zitumikapo kama taswira katika kazi za fasihi hazihitaji ufafanuzi kwa kuwa zinafahamika (Beaty, Booth, Hunter na Mays, 2002).

Wataalamu mbalimbali wa sanaa wanakubali kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya sanaa na jamii. Kutokana na uhusiano huu maudhui ya kazi za kisanii huakisi mtazamo, upeo na utamaduni wa jamii. Wasanii hujikuta wakitunga kazi zinazoakisi jamii kwa kudhamiria au kutodhamiria (Blommaert, 2006). Muziki wa Bongo Fleva, kama zilivyo sanaa zingine, hauna uwezo wa kupingana na ukweli huo. Kutokana na athari hizo muziki wa Bongo Fleva huzungumzia masuala mbalimbali yanayohusu jamii kijamii, kiuchumi na kisiasa (Omari, 2009). Athari hizo zinatokana na sababu mbalimbali zikiwemo zile zinazohusisha aina ya muziki ambayo mara nyingi huenda sambamba na maudhui ya muziki wenyewe. Kwa mfano, wasanii wengi wa muziki wa kufokafoka hujitambulisha kwa kudai haki na kukemea uovu wa aina yoyote ile katika jamii.

Wafeministi mbalimbali wanaamini kuwa uana wa kike na uana wa kiume ni dhana ya kibayolojia, lakini jinsia ya kike na ya kiume inatokana na makuzi ya kila siku katika familia na jamii kwa ujumla (Oyewumi, 2011). Kama kawaida sanaa huakisi masuala mbalimbali yanayotokea katika maisha ya kila siku. Jamii inapobadilika sanaa vilevile hubadilika kwa sababu sanaa huathiri na huathiriwa na jamii (Vazquez, 1973). Baadhi ya nyimbo za Bongo Fleva huzungumzia masuala yapatikanayo katika jamii nyingi za kiafrika hasa zile zenye kiwango kikubwa cha mfumodume. Katika jamii za aina hii mwanamke anachukuliwa kama mtu wa daraja la chini kuliko mwanaume kiasi cha wazazi kumpenda zaidi mtoto wa kiume (Izugbara, 2004). Mwanamke anachukuliwa kama kiumbe cha kumstarehesha mwanaume kingono.

Suala jingine linalojitokeza katika nyimbo za Bongo Fleva ni matumizi ya uume kama silaha ya kumnyanyasa mwanamke. Mwanamke anapochukuliwa kuwa kahaba kwa kuhusiana kingono na wanaume wengi, wanaume wanaohusiana na wanawake haohao hawaonekani kama wanaotenda maovu kama anavyoonekana mwanamke. Tendo la ngono kwa mwanaume huonekana la kishujaa wakati kwa mwanamke tendo hilo huonekana kuwa la aibu. Mawazo haya yanapatikana katika nyimbo za Bongo Fleva za *Vocha* na *Dege*. *Vocha* hutumiwa na binadamu kwa lengo la kuweka fedha kwenye simu kwa ajili ya mawasiliano. Kabla ya kukwanguliwa vocha ina thamani kubwa lakini ikishakwanguliwa na kutumika hutupwa. Huu ndio mtazamo wa wanaume kama inavyodhihirika katika wimbo huu kwamba, mwanamke akishamstarehesha mwanaume anakosa thamani na hivyo hutupiliwa mbali na mwanaume kumtafuta mwingine. Taswira ya *Dege* ni hasi zaidi kwa sababu ya sifa za dege kama nomino ambazo zimefafanuliwa kwa kina katika wimbo uitwao *Dege*. Dege ni mwanamke asiyefaa katika jamii kwa sababu ana sifa za kiume ambazo ni kutojali, ulevi na mahusiano na wanaume wengi. Kutokana na sifa hizi za kiume hafai na ikiwezekana anapaswa kupigwa kwa manati. Mfumodume unaodhihirika katika nyimbo hizi umekuwepo siku nyingi ambapo umechangia wanawake kunyimwa fursa ya kujiendeleza na kujikomboa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Suala hili la taasubi ya kiume limesababisha wanawake kusalia chini ya wanaume takriban katika masuala yote ya ujenzi wa jamii. Kwa hiyo dhana ya mwanamke

kumstarehesha mwanamke imeanzia katika misingi hiyo ya kukosa uhuru kama alionao mwanaume. Taswira ya mwanamke inavyobainishwa katika Bongo Flewa inajidhihirisha pia katika uchezaji wa wanawake kwenye video (Omari, 2009). Picha za video za nyimbo za *Dege, Vocha, Samaki* na *Bata* zinawaonyesha wasichana wengi wamevaa na kucheza kwa namna ya kuchochea ngono ilhali wavulana wamevaa nguo za heshima. Hii inaakisi hadhi na nafasi ya mwanamke katika jamii kama inavyojidhihirisha katika utendaji wa sanaa mbalimbali.

Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Taarab

Zaja amechunguza nyimbo tatu za taarab ambazo ni *Tutabanana Hapa Hapa* (Mwanahawa Alley), *Nani Zaidi* (Zuhura Shaaban) na *Mtie Kamba Mumeo* (Khadija Kopa). Lengo lake lilikuwa kubaini jinsi mambo yanawekwa wazi wakati yanapaswa kuwa siri kutokana na yaliyomo katika mashairi simulizi yanayoimbwa, kurekodiwa na kusambazwa. Ametamatisha kwa kueleza kwamba uimbaji wa taarab ni njia ya kuendeleza mapambano ya wanawake dhidi ya taasubi ya kiume. Japo mawazo yake ni ya kifeministi yameonyesha kwamba swala la taasubi ya kiume linajitokeza katika nyimbo za taarab ambapo wanawake wanajizatiti kukinza nafasi ndogo wanazopewa katika jamii. Mawazo yake yamechangia katika kuchunguza kwa kina masuala ya kifeministi yanayoibuka katika jamii na ambayo yametajika katika nyimbo hizi. Kazi yetu imeshughulikia uchanganuzi na uhakiki wa matini ambayo yametumika katika nyimbo teule za taarab ili kubaini mchango wa nyimbo hizo katika kuendeleza maudhui katika jamii hususan lugha inavyomchora mwanamke.

Taswira ya Mwanamke katika Jamii za Kiafrika

Suala la ujinsia limekuzwa na watu wa Magharibi kiasi cha kuifanya dunia nzima, Afrika ikiwemo kuamini kuwa unyanyasaji wa kijinsia unaathiri maisha ya kila siku ya wanawake (Oyewumi, 1997). Oyewumi anatoa mfano katika jamii ya Kiyoruba kuwa majukumu katika jamii hii hayagawanywi kwa kuzingatia jinsia bali umri, na hilo linathibitika kwa kuchunguza lugha ya Kiyoruba. Hata hivyo anakiri kuwepo kwa unyanyasaji wa wanawake katika jamii hiyo katika tafiti zake nyingine (Oyewumi, kama hapo juu). Ukweli unabaki kuwa jamii nyingi za Kiafrika zimeathiriwa na mfumodume kwa kiasi kikubwa. Sifa za kimajukumu za mwanaume na mwanamke zimeundwa na jamii ambamo watu hawa wawili wamekulia kutokana na sababu za kimazingira. Kwa hiyo mwanamke anakuwa mwanamke na mwanaume anakuwa mwanaume kutokana na makuzi pamoja na mazingira alimokulia (Izugbara, 2004). Ukubwa na udogo wa wanawake unajitokeza kuanzia katika ngazi za familia. Hili linajidhihirisha hata katika utoaji wa majina kwa watoto. Izugbara anatoa mifano tofauti ya majina ya watoto wa kiume na watoto wa kike katika majina ambayo yanatolewa kwa misingi ya kimfumodume. Kutokana na mfumodume familia nyingi zinapendelea kupata mtoto wa kiume kuliko mtoto wa kike nchini Nigeria. Majina ya mtoto wa kiume yanawakilisha nguvu, matumaini na utimilifu. Kwa upande mwingine majina ya watoto wa kike yanaonyesha kutokukidhi kwa matarajio ya familia. Ifuatayo ni mifano ya majina ya watoto wa kiume na maana zilizomo katika majina hayo; *Obisike, Obiesiemike, Obidike* (moyo wangu umeimarika), *Ebisike* (sasa nipo imara), *Nwokedi* (hapa kuna mtu), *Obiajulu* (woga wangu umekwisha). Majina ya watoto wa kike ni pamoja na; *Ogadinma* (hali itakuwa nzuri baada ya muda mfupi), *Ndidi* (uvumilivu), *Anaelechi* (Ninamtumaini Mungu), *Anaedi* (Ninaendelea kuvumilia).

Nadharia ya Ufeministi

Ufeministi ni jina linalomaanisha ukombozi wa mwanamke huku likijumuisha aina nyingi za misimamo pamoja na matapo na itikadi zinazonuia kutetea haki za wanawake. Ufeministi hulenga kuweka wazi dhiki zinazowakumba wanawake ili kuwaengua kutokana na ubaguzi

wa kijinsia kote ulimwenguni (Beasley, Chris 1999). Ubaguzi wa wanawake umedumu kwa kipindi kirefu na umeibukia kuwa chanzo kikuu cha ukandamizwaji wao huku wakichukuliwa na jinsia ya kiume kuwa: Vyombo dhaifu, wanyonge na ambao kazi yao ni jikoni, kumtumbuiza mwanamume, kubeba uja uzito, kuzaa, kulea watoto na kufanya kazi za nyumbani zikiwemo kumtumikia mwanamume atakavyo. Miongoni mwa haki zinazopiganiwa ni upataji wa vyeo serikalini na katika mashirika mbalimbali yanayotoa ajira, kufanya kazi na kulipwa mshahara, kumiliki mali ya wazazi, ya mume au mali inayotokana na jasho lao wenyewe na ambayo ni haki yao na pia kufanya mikataba sawa na wanaume.

Nadharia hii inawatazama wanawake kama wanajamii wenye nafasi walizopewa na jamii zao kutokana na itikadi zinazoendelezwa na jamii hizo. Isitoshe, huwaona wanawake kama wanaonyanyaswa kwa misingi ya uana au jinsia yao hata katika dini kama tulivyotaja awali. Kuna kazi walizotengewa wanawake ambazo ni duni katika jamii ambapo jamii yenyewe ina mielekeo ya kutisha kuhusu wanawake. Fasihi inaweza kutupatia mwangaza kuhusu tofauti za kijinsia na kitabaka jinsi zinavyopatikana katika jamii. Uhakiki wa kijinsia huzingatia misingi ya ukandamizaji katika tabaka na pia katika mfumo unaomtukuza mwanamume na kumtweza mwanamke. Mbali na utabaka matatizo ya mwanamke yako kuumeni (Simiyu, 2011:226). Hii ina maana kwamba matatizo ya wanawake yanatokana na wanaume. Wanaume ndio kizingiti kikuu cha ukuaji wa wanawake kiuchumi kupitia kwa nyenzo hafifu zinazoenda sambamba na utamaduni pinganifu kwa mwanamke.

Uhakiki wa ufeministi ulishika nguvu katika miaka ya 1960. Kazi mbili kuu zinazorejelewa hapa ni *A Room of One's Own* iliyoandikwa na Virginia Woolf na *A Vindication of the Rights of Women* ya Mary Wollstonecraft (1792). Kazi za hawa wandishi wa kike zilikuwa na mchango mkubwa katika kuanzisha harakati za ukombozi wa wanawake. Katika kitabu cha *The Second Sex* kilichoandikwa na (Simon de Beauvoir, 1952) anashambulia na kukosoa baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdunisha mwanamke. Anakashifu utamaduni unaomtazama mwanamke katika hali ya ubaya na udhaifu huku ikimchukulia mwanamume kama binadamu kielelezo. Beauvoir anasisitiza kuwa hali ya unyonge anamojikuta mwanamke inatokana na utamaduni unaomkuza (katika Wafula na Njogu, 2007).

Mwandishi mwingine ambaye ameathiri historia ya ufeministi ni Kate Millet aliyeandika kitabu cha *Sexual Politics* (1970). Millett anabainisha kuwa miundo ya kijamii pamoja na asasi zake ndizo chanzo cha kumkandamiza mwanamke. Pia anaishambulia mikabala ya Saikolojia – Changanuzi inayohusishwa na Sigmund Freud kwa kuwa na upendeleo mkubwa wa mfumo wa ubabedume. Freud alisema kuwa mtoto wa kike anaanza kujichukua anapogundua kuwa hana kiungo cha kiume, hali ambayo husababisha anachokiita 'wivu wa zubyu.' (Millet, 1970) anadahili kuwa wivu uliopo ni wa uwezo alionao mwanamume kutokana na muundo wa kijamii. Mwanamke anakuwa na wivu wa kinachoashiriwa na hilo zubyu wala sio zubyu kama kiungo cha mwili (Wamitila, 2003).

Tunapozungumzia ukandamizwaji wa wanawake ni muhimu kutambua kuwa Barani Afrika, mwanamke amezingirwa na maisha yenye vikwazo vingi tangu kale. Maisha yake ni ya jikoni, shambani na kitandani. Hali hii inarutubishwa na taasubi ya kiume ambapo mwanamke huchukuliwa kama chombo cha kumtumikia na kumburudisha mwanamume. Hii inadhihirika katika kazi za kale za Kiswahili kama vile katika *Utenzi wa Mwanakupona* Binti Mshamu (Mulokozi, 1999). Mwanakupona anapomshauri binti yake kwa jina Mwana Hashima Binti Sheikh kumtii mume wake anasema hivi:

Ubeti wa 24:

*Na awe radhi mumeo
Siku zote mkaao
Siku mukhitariwao
Awe radhi mekuwia*

- Ubeti wa 25:** *Na ufapo wewe mbee
Radhi yake izegee
Wende uitukuzie
Ndipo upatapo ndia*
- Ubeti wa 26:** *Siku ufufuliwao
Nadhari ni ya mumeo
Taulizwa atakao
Ndilo takalotendewa*
- Ubeti wa 27:** *Kipenda wende peponi
Utakwenda dalhini
Kinena wende motoni
Huna budi utatiwa*

Ubeti wa 24: Mwana Hashima anashauriwa kukaa vizuri na mume wake ili kila mara awe amemuwia radhi hivi kwamba (ubeti 25) akitangulia kufa basi mumewe atakuwa ameshamswafia njia. Wakati wa ufufuo mumewe ndiye atakayeamua awekwe wapi, peponi au motoni (ubeti wa 27).

Mwanakupona anamwambia kuwa mumewe akitoka aagane naye na akiingia amkaribishe na kumtengenezea pa kupumzikia.

- Ubeti wa 30:** *Kitoka agana naye
Kingia mkongowee
Kisa umtengezee
Mahala pa kupumua*

Katika beti nyingine za utenzi huu (beti 33, 34, 35) Mwanakupona anamtaka Hashima amtayarishie mumewe kiamsha kinywa kizuri, amkoshe, amnyoe ndevu na kumtunza kama mtoto mdogo asiyejua chochote. Lakini baada ya wema huu wote Mwanakupona anasema mumewe Hashima akimlipa haya mema yote kwa mabaya asijitete kwa sababu Mwenyezi Mungu atamlipia (Mulokozi, 2002: 123-140).

Utenzi huu ni muhimu kwa wanaufeministi wanaopinga majukumu mengi anayowajibika mwanamke kuyafanya na ambayo yanatokana na itikadi na mifumo ya jamii mbalimbali za kiafrika. Mume anadekezwa kama mtoto hasa katika masuala ya ndoa ili afanyiwe kila kitu na mkewe, lakini katika masuala mengine mathalan ya urithi anawekwa mbele ili mwanamke asipate chochote.

Huu ni utungo ambao uliandikwa na mwanamke na ukitazamwa katika msingi wa jamii za wakati huu unaendeleza itikadi hiyo ya ki-babedume. Lengo kuu la ufeministi ni kuibusha njia na mbinu za kutazamia kazi mbali mbali za fasihi ili kuiangazia mitazamo ya wanawake na thamani zao (Khatib, 1985).

Ufeministi wa Kiislamu umepiga hatua kubwa mbele ukiulinganisha na ufeministi wa kimagharibi kwa sababu, wakati ambapo ufeministi wa kimagharibi ulidai haki ya mwanamke katika nyanja za umma kazini, elimu na kadhalika, ufeministi wa kiislamu umedai haki hizo na uadilifu kwa mwanamke mpaka nyumbani kwake hususan katika ndoa na mahali popote anapotangamana na wanaume. Nadharia ya ufeministi wa kiislamu humwangukia mwanamke kwa heshima, usawa, haki na taadhima na inajikita kwenye usawa wa viumbe wote, wake kwa waume (Ogechi na wengine, 2008).

Mihimili Mikuu ya Nadharia ya Ufeministi

Ufeministi ni tapo linalolenga kuleta usawa katika masuala ya utamaduni na uana ambapo linapigania jamii mpya yenye misingi katika amali za kibinadamu. Amali hizo ni za kike na za kijadi miongoni mwa nyingine na ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa. Tapo hili hutumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kiyakinifu hali anamojikuta mwanamke ili kuwawezesha watu wengine kuelewa hali hiyo. Mwanamke hujikuta amepuuzwa katika masuala ya ujenzi wa taifa huku majukumu yake yakionekana kuwa ya kawaida na mepesi. Usawa unakosa kuwepo pale ambapo mwanamume anachorwa kuwa mwamuzi wa maisha ya familia nzima hata pale anaposhindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na wadhifa anaopewa na jamii (Wamitila, 2002).

Ufeministi ni tapo linalojaribu kukuza na kuendeleza hisia za umoja kati ya wanawake ili waweze kupendana na kuondoa dhana ya kuwa wanawake hudhulumiana wenyewe kwa wenyewe. Vilevile ni mtazamo unaonua kuzindua mwamko kwa upande wa jinsia ya kike wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine.

Mtazamo Mpya wa Mwanamke katika Wimbo -“Sina Muda Huo.”

Mtunzi wa taarab ya *Sina muda huo* Leyla Rashid amezungumzia suala la matumizi mazuri ya muda. Mtunzi huyu amewagusa mama wengi ambao wamekuwa wakiutumia muda wao kusengenyana badala ya kujishughulisha na kazi ya kuwaingizia kipato. Ametoa funzo kwa wanawake wajipe shughuli za kuwajenga kiuchumi kwa kusaka tonge akimaanisha watafute riziki. Anasema:

*Huna kazi si ukalime, kusema usinifosi,
Hauna haya muone, funga domo usiniseme,
Niache sina nafasi, tafuta jambo jjingine,
Ila uongo usiseme, na wajinga usinimix*

Mwanamke anapewa mamlaka ya kutafuta riziki, mwimbaji anaposema:

*Naishi na washikaji, wakati sinao,
Na yangu mengi mahitaji, sina muda huo
Mimi nalisaka tonge, ili liende kinywani,
Nitajitia mazonge, kuingia mashakani,*

Mwimbaji anatambua mwamko mpya wa mwanamke wa kutaka kujitegemea. Mwanamke anasema kuwa hana wakati wa kuzubaa, sasa yeye anasaka tonge sio wa kupiga kelele ya kujiongezea dhiki.

*Niende huku, niende kule, kuitafuta riziki,
Sio kupiga kelele, kujiongezea dhiki,
Sina muda huo sina, wa kukaa vibarazani kumdiskasi mtu,
Sina muda huo, sina, wa kukaa vipembeni nimsimange mtu
Usinipikie majungu, mie si mke mwenzio
Muda huo sina wa kuchezea.*

Msanii anaongeza kusema kuwa mwanamke hana muda wa kukaa vibarazani akiwasengenywa watu. Mwanamke anatambua haki yake ya kukataa uke wenza na hivyo kukomesha tabia ya watu kusema uongo juu yake kwa kuwaambia wanawake wenzake wasimpikie majungu. Nyimbo za taarab zimejengeka kwa misingi ya dini ya Kiislamu ambayo inaruhusu mwanamume kuoa zaidi ya mke mmoja na hivyo wanawake wengi katika

ndoa hujikuta wakiwa na wake wenza. Huku mwanamume akipewa mamlaka hayo ya kuoa wake wengi, mwanamke hajaruhusiwa kuwa na wanaume zaidi ya mmoja.

Katika ubeti unaofuata mwanamke anadai kuwa ana mambo yake ya msingi ya kufanya. Anashangaa namna anavyosemwa na walimwengu wanaomsimanga.

*Nina hamsini zangu, zinanipeleka mbio,
Aloniamuru Mungu, siyamalizi kwa leo,
Iweje ya walimwengu, mie sina muda huo,
Sinipikie majungu, mie si mke mwenzio,
Vibaya usiniseme, ukanitia nuksi
Usitake tuchambane, mimi si wewe gumegume,
Iliyokujaa mikosi, ubaya tusitafutane,
Huna kazi, si ukalime, kusema usinifosi,*

Ubeti huu unawasihi wanawake badala ya kutusiana kwa chuki wafanye kazi yenye manufaa kama kwenda kulima.

*Tafadhali nakukanya, mie sina time na wewe
Jiangalie juu mpaka chini, kisha uniambie unanisumbua nini,
Mpaka nikae nikuseme pembeni,
Wewe ni wa kuambiwa nini, uso na macho,*

*Una hamu nikuseme, nikikusema utalia,
Una hamu nikuchambe, nikikuchamba utazimia,
Utabaki ati ati, la kwangu hulipati ng'oo.....
Hilo lako joto hupati baridi, maisha yako yote,*

Katika beti hizi mbili mwimbaji anamchora mwanamke ambaye hana muda na mwenzie mwenye umbea. Anasema haoni sababu ya kujishughulisha na huyo mdaku ambaye anataka tu wagombane, kisha anamkanya kwamba akigombana naye atamliza.

Mwanamke Mpya Kinyume cha Wazo Ganda la Umbea

Katika jamii nyingi za Afrika ya Mashariki mojawapo ya wazo ganda kuhusu wanawake ni kwamba ni hodari katika umbea na masimango. Umbea ni maudhui makubwa katika nyimbo za taarab. Ni vigumu kupata wimbo wa taarab usiozungumzia udaku kwani umbea unahusishwa zaidi na wanawake Waswahili ambao wanapenda kusikiliza nyimbo za taarab. (Timammy, 2002) anasema wanawake hushiriki katika masengenyo na vijembe hutawala wanapokuwa katika sherehe za harusi au hafla mbalimbali za kijamii. Kwa kuwahusisha wanawake na tabia ya umbea, wanaume ambao wanatunga nyimbo kama hizi wanamsawiri mwanamke kama mtu ambaye kazi yake ni umbea kuhusu watu wengine na hasa wanawake wenzake kuhusu mavazi na vipodozi wanavyotumia. Katika ubeti ulio hapa chini mwimbaji anamchora mwanamke ambaye hana nafasi ya masimango:

*Sina muda huo, sina, wa kukaa vibarazani kumdiskasi mtu
Sina muda huo, sina, wa kukaa vipembeni nimsimange mtu*

*Una hamu nikuseme, nikuseme utalia
Una hamu nikuchambe, nikuchambe utazimia
Cha kunishughulisha kwako mie sikioni
Niangularie juu mpaka chini uniambie*

Beti hizi mbili zinaeleza kuwa mwanamke amebadilika na kuachia mbali masimango, masengenyo na umbea. Mwanamke anaonyesha kukomaa kifikra na kuingia katika ulingo wa kujiwezesha na ndipo hana muda wa kukaa vibarazani kumsema au kukaa vipembeni kumsimanga mtu. Anatoa tahadhari kwa anayetaka umbea kwamba akimsema atalia, na akimchamba akiwa na maana ya kumtukana, atazimia. Hapa mwanamke anaashiria kuwa na tajriba kubwa katika masuala hayo ya kuchokozana kiasi cha kumliza mwenzie na hata kumfanya azimie.

Mwanamke Mpya Udi wa Kuheshimiwa

Wimbo wa *Chози la Mama* ulitungwa na Mzee Yusufu ingawa sasa hivi mtunzi huyu amejitenga na ulingo wa muziki wa taarab. Wimbo huu umejikita katika kuzungumzia upendo kwa mama na kumchora mama kama ‘kitu’ chenye thamani sawa na manukato. Msanii anawahimiza watoto kumheshimu mama. Mzee Yusufu anasema kwamba mtoto asipomheshimu mama atakosa radhi na kwamba kumpenda mama ni rai na si kumwacha kwani huenda mtoto akapata laana. Mwimbaji anasihhi heshima kwa mwanamke kwa kutongoa hivi:

*Ni laana Chози la Mama likidondoka, kwa sababu zisizomaana,
Kakulea akakufunza, vyenye raha akajinyima na tabia akakufunza
Hili baya na hili jema na bado unamkwaza, badala ya kumtendea wema
Kwa amri ya muweza, mpende mara tatu mama kichumpa!*

Ubeti wa kwanza unaonyesha majukumu ya mama yakiwa kulea watoto na kuwafundisha maadili huku akijinyima vitu vya raha. Kwa sababu hizi watoto wanashauriwa kutomkwaza na badala yake atendewe mema.

*Si kama, si kama baba hafai, heshima yake nampa kwa kuwa na nguvu yake
Ila mama, ila mama haifai, sumu na shida kumpa,
Kwa kifupi hali yake! Kumheshimu ndio rai,
Si kumwacha na kusepa kumtunza ni haki yake, huwezi ukajidai
Na huku unanenepa, mama dhofu hali yake
Kumheshimu ndio raiiii, sikumuacha na kusepa*

Katika ubeti wa pili nasaha ya kumheshimu baba na kumtunza mama inatolewa ambapo suala la usawa kati ya wazazi wote wawili linajitokeza. Mwimbaji anaonya dhidi ya kusepa na kumghaya mama ili ahangaike. Anapozungumzia nafasi ya mwanamke inavyotetewa katika nyimbo za taarab kule Zanzibar anasema kwamba mwanamke asichorwe kama asiyefaa na asiyetunzwa bali iweze kudhihirika wazi kwamba mwanamke ni sawa na udi na ni wa maana hivyo anapaswa kuwekwa kwenye kiwango kimoja cha maslahi sawa na mwanamume (Yego, 2011).

*Hili jambo halifai, mimi hili nalikwepa
Lisitoke chozi lake, madhali mama yu hai,
Kaa chini yake kwamba, uzipate radhi zake.*

Ubeti wa tatu unaashiria kwamba mama ni muhimu katika maisha ya mtu kwa sababu usipokaa chini yake ukamheshimu atatoa chozi lake na hivyo utalaaniwa.

Sitaki radhi kukosa, likitoka chozi lake kwa sababu zisizomaana

*Sumu mama kumtesa, hata kosa liwe lake, Mzazi hakosei mwana.
Pale makavu tikisa, mama anatoa chake ili amsitili mwana,
Tunayafanya makosa mtu akipata chake, anamuona hana maana*

Katika ubeti wa nne mwimbaji anasema ni sumu kumtesa mama kwa sababu hamkosei mwana. Anaonya kuwa mtoto anapokuwa na mahitaji mama humtimizia lakini mtoto anapopata chake humdharau mama na hilo ni kosa kubwa. Katika wimbo mzima mwimbaji anazungumzia kitendo cha kudharau ambacho kinaeleza hulka ya watoto kuwaasi kina mama na anafafanua kwamba mtoto atapata athari ya kukosa radhi ya mama. Tunaona mwamko mpya wa msisitizo wa heshima kuelekezwa kwa mama mzazi na anayetilia mkazo huu akiwa ni mwimbaji wa kiume. Hili ni jambo ambalo linashughulikiwa na wanaufeministi kuhusu mwanamke, kwamba, anastahili heshima sawa na mwanamume. Katika wimbo huu mwimbaji anadai kuwa baba anapewa heshima ila mama pia asipate shida. Anasema ni haki ya mama kutunzwa asiachwe kuteseka huku baba akinenepa. Maoni haya yanatokana na mateso wanayopitia kina mama kutoka kwa wanaume ambao wametawala maisha ya wanawake. Wimbo huu unajaribu kuunga mkono jitihada za wanaufeministi za kumuweka mama sawa na baba katika masuala ya ndoa ambapo heshima inahitajika kati yao wawili.

Hitimisho

Katika makala hii tumechunguza nyimbo mbili zilizoimbwa na bendi ya *Jahazi Modern Taarab* (JMT) kwa kuzingatia mkabala wa kifeministi. Wimbo wa kwanza unasema *Sina Muda Huo*. Mwanamke amejitahidi kujikomboa kutoka minyororo ya utamaduni gandamizi inayopinga juhudi zake za kuwa sawa na mwanamume. Ameamua kuacha udaku, masimango na masengenyo ili kutafuta riziki na hivyo hana muda wa kuchambana na wenzake. Hatua hii inamwonyesha mwanamke kama kiumbe ambaye ametambua uwezo wake wa kutekeleza majukumu sawa na mwanamume na wala si kubaki tu jikoni akifanya kazi za nyumbani na shambani. Wimbo wa pili ni *Chizi la Mama* na unasisitiza heshima na mapenzi kwa mama. Watoto wanashauriwa kumheshimu mama na baba anashauriwa kumtunza mama ili yeye baba asinenepe wakati mama anadhoofika na kukonda. Basi tunaweza kuhitimisha kwamba nyimbo za taarab ambazo tumezichunguza zinachangia ukombozi wa mwanamke kutokana na majukumu ya kiubaguzi na mawazo ganda katili kumhusu mwanamke. Mwanamke wa kisasa anapigania haki na usawa kutoka kwa asasi zinazomkandamiza huku jamii ikihamasishwa kutambua suala zima la ukwezwaji wa jinsia ya kike.

Marejeleo

- Askew, K. M. (2002) *Performing the nation-Swahili music and cultural politics in Tanzania*. USA, Chicago: University of Chicago Press.
- Beatty, J., Booth, A., Hunter J.P. Mays, K. J. (wah.) (2002) *The norton introduction to literature (8th Edition)*. New York: W.W. Norton & Company.
- Blommaert, J. (2006) Applied ethnopoetics. *Narrative Inquiry* 16(1): 181-190.
- Birke, L. (1986) *Women, feminism and biology: The feminist challenge*. Brighton; Wheatsheal.
- Cuddon, J. A. (1991) *Penguin dictionary of literacy terms and literacy theory*. London: Penguin.
- de Beauvoir, S. (1952) *The second sex*. Trans. H.M. Parshley. New York: Modern Library.
- Halliday, M. A. K (1985) *An introduction to functional grammar*. London & New York: Routledge, Francis & Taylor Group.
- Igobwa, S. E. (2007) *Taarab and chakacha in East Africa: Transformation, appreciation and adaptation of two popular music genres of the Kenyan coast*. Paper presented during conference on Music in the world of Islam, 8-13 August, 2007, Toronto, Canada.

- Izugbara, C. O. (2004) *Patriarchal ideology and discourses of sexuality in Nigeria*. Understanding Human Sexuality Seminar Series 2. Africa Regional Sexuality Resource Centre.
- Khamis, S. A. M. (2002) Wondering About Change. *Nordic Journal of African Studies* 11, pp 198-205. Helsinki: Nordic association of African studies.
- Khatib, M. S. (1992) *Taarab in Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Khatib, M. S (1985) Utendi wa mwana kupona. *Mulika* 17: 46-52.
- Matei, A.K. (2014) *Discourse, gender identity and gender power relations in fiction: A CDA and SFL reading of Wamitila's unaitwa nani?* Unpublished PhD Thesis: University of Nairobi, Kenya
- Mgana, I. (1991) *Jukwaa la Taarab Zanzibar*. Helsinki: Medi Africa.
- Mlaga, W. K. (2017) *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi. Karne Ya 21*. Heko Publishers Ltd.
- Mulokozi, M. M. (MH) (1999) *Tenzi tatu za kale*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.
- Nagel, J. (2003) *Race, Ethnicity and sexuality: intimate intersections, forbidden frontiers*. New York: Oxford University Press.
- Nyenembe, J. (1997) *Jinsia Upeo wa wanaume na wanawake*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Ogechi, O. N, Shitemi, L.N., na Simala, K. I. (wh) (2008) *Nadharia katika taaluma ya Kiswahili na lugha za kiafrika*. Moi University Press.
- Omari, S. (2009) *Tanzanian hip hop poetry as popular literature*. Unpublished PhD Literature Thesis. University of Dar es Salaam, Tanzania.
- Omari, S. Mrikaria, G (wah) (2010/2011) *Toleo maalum la muziki wa kizazi kipya: MULIKA NA.29 &30*. Taasisi ya Taaluma Ya Kiswahili. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Oyewumi, O. (1997) *The invention of women: Making an African sense of western gender discourses*. Minneapolis: University of Minnesota Press.
- Oyewumi, O. (2011) Introduction. In Oyeronke Oyewumi (Ed.) *Gender epistemologies in Africa. Gendering traditions, spaces, social institutions and identities* (pp. 1-7). New York: Palgrave Macmillan.
- Timammy, R. (2002) *Mombasa Swahili women's wedding songs*. University of Nairobi: Unpublished PhD Thesis, Kenya.
- Vazquez, A.S. (1973) *Art and society: Essays in marxist aesthetics*. London: Merlin Press.
- Wollstonecraft, M. (1792) *A vindication of the rights of woman*. Boston: Peter Edes.
- Woolf, V. (1929) *A room of ones own*, 52 Tavistock Square, London. Hogarth Press.
- Wafula R. M. Njogu K. (2007) *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya fasihi. Istilahi na nadharia*. Nairobi. Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa fasihi. Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Yego, E. K. (2011) *Nafasi ya mwanamke: Jinsi inavyotetewa katika nyimbo za taarab Zanzibar: Tasnifu ya shahada ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi*. Haijchapishwa.
- Simiyu, W. F. (2011) *Kitovu Cha fasihi simulizi*. Serengeti Bookshop. Mwanza, Tanzania.
- TUKI (2014) *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Dar Es Salaam. TUKI.
- Zja, J. O. (2008) *Publicizing the Private: Feminist locution in taarab songs and performance*. A Paper presented at the CODESRIA 12th General Assembly on 7th-11th Dec 2008. Yaounde.